



AB. 278/349/01/36

**TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA
AMRI YA SERIKALI JUU YA VYAMA VYA USHIRIKA
SHERIA YA VYAMA VYA USHIRIKA Na.6 YA MWAKA 2013**

**Yah: TAARIFA YA UTEUZI WA WAFILISI 158 KWA AJILI YA KUFILISI VYAMA VYA
USHIRIKA 2,320 TANZANIA BARA VILIVYOFUTWA MWEZI JULAI, 2022**

Mimi **Benson Otieno Ndiege** Mrajis wa Vyama vya Ushirika nimeridhika kuwa Vyama vya Ushirika 2,320 vya Tanzania bara vimeshindwa kufanya kazi zake katika kutimiza Masharti ya usajili wa Vyama hivyo ikiwa ni pamoja na kuacha kufanya kazi kwa muda mrefu.

Kutokana na sababu hizo, na kwa mamlaka niliyopewa chini ya kifungu cha 100 (2) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013 nilivifuta Vyama hivyo kwenye Daftari la Serikali la Vyama vya Ushirika na kwa mujibu wa kifungu cha 103 (1) (b) cha Sheria hii, nimewateua **wafilisi 158** kufanya ufilisi wa Vyama kulingana na orodha iliyoambatishwa. Uteuzi huu utanza tarehe ya taarifa hii kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

Imetiwa saini na mimi hapa **Dodoma** leo siku ya **Jumanne** tarehe **nne Mwezi Oktoba** Mwaka **elfu mbili na ishirini na mbili**.

Dkt. Benson O. Ndiege

MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA